**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MKOA WA LINDI

## MWONGOZO WA UNUNUZI WA MAZAO YA UFUTA NA MBAAZI KWA KUTUMIA MFUMO WA STAKABADHI YA GHALA

**MSIMU 2021**


***Imeandaliwa na:-***

***Ofisi ya Mkuu wa Mkoa***

***S.L.P 1054***

***LIND***

# YALIYOMO


**VIFUPISHO....................................................................................................4**

**DIBAJI ........................................................................................................5**

**SEHEMU YA KWANZA .....................................................................................7**

**1.UTANGULIZI ..............................................................................................7**

**SEHEMU YA PILI ..........................................................................................10**

**2.0MFUMO WA UKUSANYAJI NA UNUNUZI WA UFUTA NA MBAAZI MSIMU WA MWAKA 2021 ...............................................................................................10**

**2.1MFUMO WA UKUSANYAJI WA UFUTA MSIMU 2020 ...........................................10**

**2.1.1 MFUMO UNAOPENDEKEZWA KWA MSIMU 2021 ..........................................10**

**2.2 MFUMO WA UKUSANYA WA MBAAZI MSIMU 2020 ...........................................10**

**MFUMO UNAOPENDEKEZWA KWA MSIMU 2021 .................................................10**

**SEHEMU YA TATU ........................................................................................11**

**3.0 WADAU**....................................................................................................11

**SEHEMU YA NNE.........................................................................................10**

**4.0 MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI ........................................................12**

**OFISI YA MKUU WA MKOA..............................................................................12**

**4.1 OFISI YA MKUU WA WILAYA**.............................................................13

**4.2 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA**.........................................................13

**4.3 VYAMA VIKUU** .....................................................................................14

**4.4 VYAMA VYA USHIRIKA VYA MSINGI.** ..................................................15

**4.5 WAKULIMA.** .........................................................................................16

**4.6 WAMILIKI/WAENDESHA GHALA** .........................................................17

**4.7 WANUNUZI/WAFANYABIASHARA/MAWAKALA.** ........ 18

**4.8 WAKALA WA VIPIMO.** ........ 19

**4.10 TAASISI ZA FEDHA.** ........ 20

**4.11 WASAFIRISHAJI.** ........ 20

**4.12 KAMATI ZA USALAMA MKOA/WILAYA ........ 20**

**4.13 BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA ........ 21**

**4.14 SOKO LA BIDHAA TANZANIA ........ 21**

**4.15 WIZARA YA KILIMO ........ 22**

**SEHEMU YA TANO ........ 23**

**5.0MAANDALIZI NA MAHITAJI KATIKA MSIMU 2021 ........ 23**

**5.7 TARATIBU ZA MINADA** ........ 27

**5.8 TARATIBU ZA MALIPO** ........ 28

**5.9 TARATIBU ZA UTOAJI WA UFUTA NA MBAAZI GHALANI** ........ 29

**SEHEMU YA SITA........ 27**

**6.1 UDHIBITI WA UTOROSHAJI/UDANGANYIFU NA UNUNUZI HOLELA WA UFUTA/MBAAZI........ 30**

**6.2 ADHABU KWA MFANYABISHARA ATAKAYEKWEPA KULIPA TOZO** ........ 30

**6.3 MNUNUZI KUCHELEWA KULIPA AU KUTOLIPA.** ........ 30

**6.4 UDANGANYIFU UNAOFANYWA NA MAKARANI AU WATENDAJI WA AMCOS.** 31

**SEHEMU YA SABA** ........ 32

**7.1 MAPENDEKEZO YA TOZO ........ 32**

**7.2 KINGA YA DHAMANA........ 33**

## VIFUPISHO

1. AMCOS – Agricultural Marketing Co-operative Society
2. BOT- Bank of Tanzan
3. GRN – Good received Note
4. PDN – Produce Delivery Note
5. TMX – Trade Market Exchange
6. TBS- Tanzania Bureau of Standard
7. BD – Bila Daraja
8. WMA- weight and Measurement Angency

# DIBAJI



Ufuta na mbaazi ni miongoni mwa mazao ya kibiashara yanayolimwa katika mkoa wa Lindi na kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni. Mkoa wa Lindi ndio unaoongoza kwa uzalishaji mkubwa wa ufuta hapa nchini. Kiasi kikubwa cha ufuta ghafi unaozalishwa uuzwa nje ya nchi na kiasi kidogo kinachobaki hutumika ndani ya nchi.

Katika kipindi cha msimu ya mwaka 2018 na 2019 mkoa ulikuwa unatumia mfumo wa ununuzi wa zao la ufuta kwa njia ya minada, ambapo ufuta ulikuwa unakusanywa na kuuzwa kupitia ghala ndogo za AMCOS ambazo hazijasajiliwa na Bodi ya leseni za ghala.
Aidha kwa msimu wa mwaka 2020 mkoa umetumia mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo mazao yalikusanywa kwenye ghala ndogo za AMCOS na baadae kusafirishwa kwenda ghala kuu za minada. Mfumo huu umeonesha mafanikio makubwa katika uuzaji na udhibiti wa upotevu wa mazao ya wakulima.

Aidha, kutokana na mafanikio yaliyopatikana kutokana na uuzaji wa mazao haya kwa njia ya stakabadhi ghalani Mkoa bado unasistiza matumizi ya mfumo huo kuendelea kutumika msimu wa mwaka 2021. Mkoa umeandaa mwongozo utakaotumika katika ununuzi wa mazao ya ufuta na mbaazi katika Mkoa wa Lindi kwa kutumia mfumo rasmi wa stakabadhi ya ghala unaosimamiwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala. (Mwongozo Namba 9 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Sekta Ndogo ya Ufuta - TOLEO Na 4 {Chini ya Kifungu cha 6 (k, l, m na o) cha Sheria Namba 10/ 2005 na Kifungu cha 6(n) cha Sheria Namba 3/2015}).

Mwongozo huu, umeandaliwa kwa lengo la kutatua changamoto zilizojitokeza kwa vipindi vya misimu iliyopita hususani ubora wa mazao yenyewe, upatikanaji wa takwimu za mauzo, ongezeko la thamani ya mazao, usafirishaji kwa wanunuzi kutoka kwenye ghala za AMCOS, udogo wa ghala za AMCOS na uadilifu wa baadhi ya wadau na viongozi kwenye AMCOS. Aidha, mwongozo huu unatoa maelekezo ya namna na

utaratibu wa usimamizi wa masoko na mauzo ya ufuta na mbaazi ghafi katika Mkoa wa Lindi na kuhakikisha kila mdau anashiriki kikamilifu, lengo likiwa kuhakikisha mkulima ananufaika na taifa kwa ujumla.

Ni matarajio ya mkoa kuwa wadau wote wanaohusika na mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya ufuta na mbaazi mkoa wa Lindi watazingatia mwongozo huu kama dira ya kufikia malengo tuliyojiwekea. Mkoa utaendelea kuboresha mwongozo huu kwa kuzingatia sera za nchi zilipo na matakwa ya kisheria na miongozo inayotambuliwa na serikali pamoja na maoni na michango ya wadau ndani ya mkoa. Ofisi ya mkuu wa mkoa itatoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha wadau wote wanashiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya mkulima mmoja mmoja, Mamlaka za serikali za Mitaa, wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla.

Ahsanteni sana.

Godfrey W. Zambi

**MKUU WA MKOA WA LINDI**

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu wa mwaka 2021 unatoa maelekezo ya namna na taratibu za usimamizi wa masoko na mauzo ya ufuta na mbaazi ghafi. Lengo ni kuona kila mdau katika nafasi yake anashiriki kikamilifu na kuhakikisha mazao ya ufuta na mbaazi yanawanufaisha wakulima, serikali za mitaa, mkoa na taifa kwa ujumla. Aidha, Mkoa pamoja na taasisi zingine za serikali zinazohusika na masuala ya kilimo na masoko ya mazao wana wajibu wa kutoa taarifa juu ya upatikanaji wa ufuta na mbaazi ghafi na kusimamia utekelezaji wa mfumo mzima ikiwemo kutoa miongozo mbalimbali.

Aidha, mwongozo una lengo la kuwaunganisha wadau wa zao la ufuta na mbaazi wakiwemo Wizara ya Kilimo na taasisi zake kama Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zake kama vile Bodi ya usimamizi wa stakabadhi za ghala, mkoa, wilaya na mamlaka za serikali za mitaa, wakulima, vyama vya ushirika, wasafirishaji, wanunuzi, waendesha ghala, taasisi za kifedha na taasisi zingine, kuhakikisha zao la ufuta na mbaazi yanaleta tija kwa mkulima na taifa kwa ujumla.

Kwa msimu huu wa mwaka 2021 Mwongozo huu pia umezingatia mfumo rasmi wa stakabadhi ya ghala unaosimamiwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala. (Mwongozo Namba 9 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Sekta Ndogo ya Ufuta - TOLEO Na 4 {Chini ya Kifungu cha 6 (k, l, m na o) cha Sheria Namba 10/ 2005 na Kifungu cha 6(n) cha Sheria Namba 3/2015}).

### 1.1 MALENGO YA UKUSAYAJI WA UFUTA NA MBAAZI GHAFI KWA MSIMU WA MWAKA 2021

#### 1.1.1 UKUSANYAJI WA UFUTA

Kwa msimu uliopita wa mwaka 2020 mkoa ulikusanya na kuuza ufuta ghafi kwa njia ya minada kupitia vyama vya ushirika jumla ya kiasi cha **kilo 62,284,032**.

Aidha, kwa msimu huu wa mwaka 2021 Mkoa unatarajia kukusanya kiasi cha **kilo 68,500,000** za ufuta ghafi kupitia vyama vya ushirika. Jumla ya vyama vya msingi 149 vitashiriki katika zoezi la ukusanyaji na uuzaji wa ufuta na ghafi kwa msimu huu wa

mwaka 2021. Pia vyama vikuu vya ushirika vitahusika katika kuratibu na kusimamia zoezi la mauzo ya ufuta kupitia minada. Vyama hivyo ni Chama Kikuu cha Ushirika cha **LINDI MWAMBAO** ambacho kinajumuisha AMCOS 52 zilizopo katika Manispaa ya Lindi, halmashauri ya wilaya ya Lindi (Mtama) pamoja na halmashauri ya wilaya ya Kilwa. Chama Kikuu cha Ushirika cha **RUNALI** kinachojumuisha AMCOS 97 zilizopo katika halmashauri za wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale.

***Jedwali Na. 01: Makisio ya uzalishaji Ufuta msimu 2021***

| NA. | HALMASHAURI | MAKUSANYO 2020 (KILO) | IDADI YA AMCOS ZITAKAZOSHIRIKI 2021 | MAKISIO 2021(KILO) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Lindi | 1,292,922 | 11 | 3,500,000 |
| 2 | Lindi Vijijini | 9,072,777 | 19 | 8,000,000 |
| 3 | Kilwa | 17,161,129 | 22 | 19,000,000 |
| 4 | Ruangwa | 12,043,395 | 27 | 13,000,000 |
| 5 | Nachingwea | 10,300,321 | 37 | 12,000,000 |
| 6 | Liwale | 12,413,488 | 33 | 13,000,000 |
| | **JUMLA** | **62,284,032** | **149** | **68,500,000** |

### 1.1.2 UKUSANYAJI WA MBAAZI

Kwa msimu wa mwaka 2020 mkoa wa Lindi ulikusanya na kuuza kiasi cha kilo **5,038,093** ambazo zilikusanya na kuuzwa mnadani. Chama kikuu lindi Mwambao waliuza **kilo 89,648** na Chama kikuu cha RUNALI waliuza **kilo 4,764,262**.

Aidha, kwa msimu huu wa mwaka 2021 mkoa umelenga kukusanya **kilo 33,378,000** za mbaazi ghafi zitakazokusanywa kupitia vyama vya ushirika. Jumla ya AMCOS 136 itahusika katika ukusanyaji na uuzaji wa mbaazi kwa msimu wa 2021. Vyama vikuu vitahusika na kuratibu minada kwa mfumo wa stakabadhi ya ghala.

***Jedwali 02: Makisio ya uzalishaji wa mbaazi msimu 2021***

| S/N | **HALMASHAURI** | **MAKUSANYO MSIMU 2020** | **MAKSIO MSIMU 2021** |
|---|---|---|---|
| 1 | LINDI VIJIJINI | 89,648 | 4,933,000 |
| 2 | LINDI MANISPAA | 0 | 1,693,000 |
| 3 | NACHINGWEA | 3,077,634 | 4,545,000 |
| 4 | RUANGWA | 1,666,164 | 11,176,000 |
| 5 | LIWALE | 204,647 | 6,706,000 |
| 6 | KILWA | 0 | 4,325,000 |
| | **JUMLA** | **5,038,093** | **33,378,000** |

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MFUMO WA UKUSANYAJI NA UNUNUZI WA UFUTA NA MBAAZI MSIMU WA MWAKA 2021

### 2.1 MFUMO WA UKUSANYAJI WA UFUTA MSIMU 2020

Katika msimu wa mwaka 2020 mfumo uliotumika ulikuwa ni wa kukusanya ufuta kwenye ghala ndogo za AMCOS na baadae kusafirishwa kwenda ghala kuu za minada.

#### 2.1.1 **MFUMO UTAKAOTUMIKA KWA MSIMU 2021**

Kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kutumia ghala kuu za minada. Mfumo huo utaendelea kutumika ili kuendelea kuwajengea wadau wote uelewa juu ya mfumo huo. Lengo kubwa likiwa ni kulinda ubora wa zao lenyewe, urahisi wa upatikanaji wa takwimu za mauzo zilizo sahihi, ongezeko la thamani ya mazao.

### 2.2 MFUMO WA UKUSANYA WA MBAAZI MSIMU 2020

Aidha, pia kwa upande wa zao la mbaazi mfumo uliotumika msimu wa 2020 wakulima walikusanya mbaazi kwenye vyama vya msingi nan a baaadae kusafirishwa kwenda ghala kuu za minada.

#### MFUMO UTAKAOTUMIKA KWA MSIMU 2021.

Kwa msimu huu wa 2021 ununuzi wa mbaazi ghafi mfumo utakotumika ni mfumo wa stakabadhi ghala, hii ni kutokana na baaadhi ya mafanikio yalipatikana kwa msimu uliopita ikiwemo; upatikanaji wa takwimu za mauzo na uzalishaji, kuanza kuimarika kwa bei. Hivyo, kwa msimu huu wa mwaka 2021 mbaazi ghafi zitakusanywa kwenye ghala ndogo za AMCOS na baadae kusafirishwa kwenda ghala kuu kwa ajili ya minada. Vyama vikuu vitaratibu minada ya kawaida kama inavyofanyika kwenye mazao la ufuta na korosho.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 WADAU

Katika mfumo wa uuzaji wa ufuta/mbaazi kwa njia ya stakabadhi ya ghala/mnada wadau watakaoshiriki watakuwa ni;-

(i) Ofisi ya mkuu wa mkoa
(ii) Ofisi za wakuu wa wilaya
(iii) Mamlaka za serikali za mitaa
(iv) Vyama vikuu vya ushirika
(v) Vyama vya ushirika vya msingi.
(vi) Wakulima.
(vii) Wanunuzi/wafanyabiashara/mawakala
(viii) Wakala wa vipimo
(ix) Taasisi za fedha.
(x) Wasafirishaji.
(xi) Bodi ya usimamizi wa stakabadhi ya ghala.
(xii) Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB).
(xiii) Taasisi ya Soko la Bidhaa (TMX)
(xiv) Waendesha ghala
(xv) Wizara ya Kilimo
(xvi) Wizara ya viwanda na Biashara
(xvii) Mamlaka ya Bandari
(xviii) Wasindikaji wa ufuta.
(xix) Benki ya Tanzania (**BOT**)
(xx) Kamati za usalama mkoa na Wilaya

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI

Katika sehemu hii ya mwongozo unataja majukumu mbalimbali ya wadau watakaoshiriki katika msimu huu wa ununuzi wa ufuta/mbaazi ghafi kwa mwaka 2021 kama ifuatavyo;

### 4.1 OFISI YA MKUU WA MKOA

Kwa kuwa mazao ya ufuta/mbaazi ghafi hadi sasa haya jakuwa na utaratibu wa kitaifa wa ukusanyaji na ununuzi wake:-

(i) Mkuu wa mkoa atakuwa ndiye msimamizi mkuu katika utekelezaji wa mfumo katika mkoa.

(ii) Sekretarieti ya mkoa itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa mfumo mzima ndani ya mkoa.

(iii) Kutoa ufafanuzi wa miongozo ya utekelezaji wa mfumo.

(iv) Kuchukua hatua za haraka katika kutatua changamoto zinazojitokeza.

(v) Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa zoezi la ununuzi wa mazao ya ufuta na mbaazi.

(vi) **Mrajis msaidizi wa mkoa:-**

a. Atakuwa mratibu mkuu wa mfumo katika Mkoa
b. Atakuwa na jukumu la kutambua AMCOS zitakazoshiriki kwenye ukusanyaji wa ufuta na mbaazi
c. Atazisimamia UNION na AMCOS namna ya ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi, uuzaji na namna ya kufanya malipo.
d. Atakuwa na jukumu la kuwasajili/kuwatambua wanunuzi wote watakaonunua ufuta na mbaazi ndani ya Mkoa wa Lindi
e. Atakuwa na jukumu la kuhakiki na kuthibiti nyaraka zote zitakazotolewa na UNIONS pamoja na AMCOS katika usafirishaji wa ufuta na mbaazi

**N.B**

**Hakuna mnunuzi atakayeruhusiwa kununua ufuta na mbaazi endapo atakuwa hajasajiliwa na kulipa kinga ya dhamana.**

a) Atakuwa na jukumu la kusimamia taratibu zote za minada
b) Atakuwa na jukumu la kusimamia taratibu zote za malipo kwa kushirikiana na maafisa ushirika wa wilaya
c) Atachukua hatua kwa vyama vya ushirika vya msingi endapo vitakiuka taratibu, sheria na kanuni kwa mujibu wa sheria ya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013 na kanuni za mwaka 2015 ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa vyombo husika.
d) Atatachukua hatua kwa wanunuzi watakaokiuka taratibu.
e) Atakuwa na jukumu la kutoa miongozo kwa nyaraka zitakazotumika wakati wa kusafirisha ufuta na mbaazi.
f) Atakuwa na jukumu la kukusanya takwimu zote za ufuta na mbaazi uliokusanywa kwenye chama cha msingi na maghala makuu pamoja na takwimu za mauzo na kutoa taarifa pale zitakapohitajika.
g) Kushirikaiana na mamlaka nyingine zinazotambulika kisheria katika kusimamia mifumo ya mauzo ya mazao kama zilivyotambukliwa na mwongozo huu.

## 4.2 OFISI YA MKUU WA WILAYA

Mkuu wa Wilaya atakuwa ndiye msimamizi mkuu katika utekelezaji wa mfumo katika Wilaya akisaidiana na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.

## 4.3 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

(i) Kusimamia utekelezaji wa mfumo katika ngazi ya wilaya.
(ii) Kuhakikisha elimu ya mfumo inatolewa kwa wakulima.
(iii) Kuhamasisha wakulima kufungua akaunti.
(iv) Kukagua na kuthibitisha maghala yatakayotumia kwa msimu wa ufuta na mbaazi
(v) Kuimarisha udhibiti kwenye vizuizi.
(vi) Kukagua nyaraka zote za usafirishaji katika maeneo yao.
(vii) Kuwagharamia watumishi wake wote wataohusika na utekelezaji wa mfumo huu.
(viii) Kudhibiti/kuhakikisha hakuna ununuzi holela wa ufuta/mbaazi ghafi kwenye maeneo wanayoyasimamia.

(ix) Kuhakiki na kudhibiti ubora katika zao la ufuta na mbaazi.

(x) Kutoa elimu kwa wakulima juu ya utunzaji wa ufuta na mbaazi baada ya kuvuna.

(xi) Kusimamia vituo vya malipo (payment centres) kwa kuhakikisha zina wataalam wa kutosha, vitendea kazi na kuwawezesha wataalam kwa kushirikiana na vyama vikuu vya ushirika.

## 4.4 VYAMA VIKUU

Vyama vikuu vitakavyoshiriki katika mfumo huu wa ununuzi wa ufuta na mbaazi kwa njia ya stakabadhi ya ghala/mnada ni **LINDI MWAMBAO** na **RUNALI** vikiwa na majukumu yafuatayo;-

(i) Kusambaza nyaraka zote zitakazotumika kupokelewa ufuta na mbaazi kutoka kwa wakulima, PDN za kusafirisha ufuta na mbaazi kwenda ghala kuu.

(ii) Kuandaa ratiba na kuendesha minada.

(iii) Kuandaa na kutoa hati ya malipo "**sales invoice"** mara baada ya mnada kwa mzabuni alieshinda tenda ndani ya masaa kumi na mbili (12)

(iv) Kuandaa vifungashio na nyaraka mbalimbali za ununuzi kwa niaba ya vyama vya Msingi ikiwa ni pamoja na usambazaji wa vitabu.

(v) Kuhakikisha vifungashio vimethibitishwa na shirika la viwango Tanzania (TBS) na alama za utambulisho kwa kila chama.

(vi) Kupokea malipo ya fedha za wakulima (AMCOS) kutoka kwa wanunuzi kupitia akaunti ya pamoja ya chama cha Ushirika (collection account).

(vii) Kuingiza malipo ya fedha za wakulima katika akaunti zao moja kwa moja.

(viii) Kufanya malipo ya wadau wengine moja kwa moja kwenye akaunti zao ikiwemo ushuru wa AMCOS.

(ix) Kutoa agizo la toleo (**Release warranty**) ndani ya masaa kumi na mbili (12) baada ya malipo kufanyika.

(x) Kutoa PDN za usafirishaji wa ufuta na mbaazi kutoka ghala kuu kwa wanunuzi

(xi) Kuandaa sales catalogue itakayotumika kwenye mnada inayoonesha, kiasi, ubora na ghala la mnada husika.

(xii) Kupokea na kutunza taarifa za stakabadhi kutoka AMCOS

(xiii) Mnunuzi atapaswa kusaini mkataba wa makubaliano wa kununua ufuta/mbaazi kwenye Chama Kikuu husika kwa mujibu wa mwongozo huu.

**4.5 VYAMA VYA USHIRIKA VYA MSINGI.**

(i) Kuhakiki na kupokea ufuta na mbaazi ghafi kutoka kwa wakulima.

(ii) Kuhakikisha ufuta uliopokelewa umekomaa vizuri, mkavu na hauna uchafu/takataka za aina yoyote.

(iii) Ufuta wa mkulima utapokelewa kwa kiwango cha **Bila Daraja (BD)** na ni lazima vigezo vifuatavyo vihakikiwe

a. Kiwango cha unyevu (mkavu)
b. Kiwango cha uchafu (foreign matter)
c. Kiwango cha mbegu zilizooza.
d. Mchanganyiko wa mbegu nyingine.

(i) Kupima na kutoa stakabadhi kwa mkulima kulingana na kiasi kilichopokelewa.

(ii) Kuhakisha ufuta/mbaazi uliopokelewa unahifadhiwa katika vifungashio maalum vilivyopendekezwa baada ya kuhakikiwa na kupimwa.

(iii) Kuhakikisha kuwa ufuta umefungashwa kwenye vifungashio ambavyo ni vipya na vilivyothibitishwa na shirika la Viwango Tanzania na kwa kuzingatia viwango vya uzito kwa mujibu wa Namba 11 la Sheria ya Vipimo na Mizani **Sura 340** iliyofanyiwa marekebisho mwaka **2002**.

(iv) Vifungashio vyote vitakavyotumika katika sekta ndogo ya zao la ufuta na mbaazi ni vile vilivyokidhi kiwango cha kimataifa ISO 23560:2015 na kuidhinishwa na Shirika la Viwango Tanzania.

(v) Uzito wa kifungashio kimoja ni **gramu 800** kikiwa na urefu wa nje wa **milimita 965** na upana wa nje wa **milimita 560.**

(vi) Uzito wa kifungashio kimoja ni **kilogramu 50.**

(vii) Kuhakikisha kuwa vifungashio vyote vina jina la mweka mali.

(viii) Kuweka alama ya utambulisho kwa kila kifungashio ikionesha jina kamili na namba yake ya usajili.

(ix) Kushirikiana na maafisa Ugani katika kusimamia ubora wa ufuta na mbaazi

(x) Kutoa PDN za usafirishaji ufuta na mbaazi kwenda ghala kuu la mnada.

(xi) Kujaza fomu za masafirisho zikionesha majina kamili ya wamiliki wa mzigo unaosafirishwa.

(xii) Kuhakikisha idadi ya vifungashio kwenye kumbukumbu za kusafirishia mazao inafanana na idadi ya vifungashio halisi vilivyopakiwa kwenye gari husika.

(xiii) Kuwa na akaunti ya malipo katika benki zilizosajiliwa hapa nchini kwa mujibu wa sheria.

(xiv) Kuandaa miamala ya wakulima na kuwasilisha kwa Maafisa Ushirika ili kuhakiki usahihi kabla ya kupeleka chama kikuu.

(xv) Kufuatilia malipo kutoka kwa vyama vikuu na benki.

(xvi) Kutunza kumbukumbu za malipo na makusanyo ya ufuta na mbaazi.

(xvii) Kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa maafisa ushirika na wadau wengine.

(xviii) Kuwasilisha tozo Chama Kikuu zinazowahusu wakulima kama zipo.

(xix) Kuhakikisha mizani zinazotumika zimekaguliwa kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo.

(xx) Kuhakikisha vifungashio vyote vimewekewa nembo na namba ya usajili wa chama husika.

(xxi) Kutoa taarifa za wakulima sehemu za wazi ili waweze kuhakiki usahihi wa taarifa zao hususani za mauzo na za kibenki.

(xxii) Kubandika taarifa za malipo ya wakulima kwenye mbao za matangazo.

(xxiii) Kubandika majina ya wakulima wote waliokusanya ufuta katika chama husika.

(xxiv) Kujaza Fomu Namba 7 iliyotolewa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala iwapo stakabadhi yoyote itabakia bila kuuzwa kwa sababu ya ufuta husika kutokuwepo ghalani (**Mis-Delivery**).

## 4.6 WAKULIMA.

kwa mujibu wa muongozo huu, wakulima watakuwa na wajibu ufuatao;

(i) Kuzalisha ufuta na mbaazi kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo.

(ii) Kuvuna, kukausha na kuweka ufuta/mbaazi katika hali ya usafi.

**NB:**

**Kuhakikisha ufuta uliopelekwa kwenye ghala za Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS) umekomaa vizuri, mkavu na hauna uchafu/takataka za aina yoyote au mchanganyiko wa mbegu nyingine**

(iv) Ufuta/mbaazi wa mkulima utapokelewa kwenye ghala za Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS) kwa kiwango cha **Bila Daraja (BD)**

(v) Kupeleka ufuta/mbaazi kwenye maghala ya chama cha Msingi cha Ushirika na kupata stakabadhi kulingana na kiasi alichowasilisha.

(iii) Kufungua na kuwasilisha akaunti Namba ya Benki iliyo hai au taasisi za fedha yenye majina yake kamili yanayotumika katika vitambulisho vinavyotambuliwa kisheria.

(iv) Kuhakiki taarifa za kibenki na kutoa taarifa kwa uongozi wa AMCOS mara atakapo ona kasoro kabla ya malipo kufanyika.

(v) Kufuatilia taarifa za mauzo ya ufuta/mbaazi wake mara kwa mara kwenye vituo vya ukusanyaji

**NB: Ni kosa kwa wakulima zaidi ya mmoja kuchangia akaunti ya Benki.**

## 4.7 WAMILIKI/WAENDESHA GHALA

(i) Ghala zote zitakazotumika kupokea na kuhifadhi zao la ufuta/mbaazi zitapaswa kukaguliwa na kusajiliwa na mamlaka husika zilizopo zinazotambuliwa na sheria.

(ii) Waendesha ghala wote watapaswa kusajiliwa na kupata leseni kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala kabla ya kuanza shughuli.

(iii) Kuzingatia sheria, kanuni na miongozo yote ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, taasisi za fedha na mamlaka nyingine za serikali.

(iv) Kupokea, kuhifadhi na kutoa ufuta/mbaazi katika ghala kwa mujibu wa mwongozo Namba 9 wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala sekta ndogo ya ufuta – TOLEO Na. 3.{Chini ya kifungu cha 6 (k,l,m na o) cha sheria Namba 10/2005 na kifungu cha 6 (n) cha sheria Namba 3/2015}

(v) Kwa makubaliano kati ya mkoa, mwendesha ghala na mweka mali, ufuta/mbaazi utapokelewa kama ufuta/mbaazi ***Bila Daraja*** na utabainishwa kwenye stakabadhi husika kwa alama **‘BD’**

(vi) Kufuata maelekezo yatakayotolewa na Mrajis Msaidizi wa mkoa au viongozi wa wilaya, mkoa au Taifa pale itakapohitajika.

(vii) Kuhakikisha vifaa vyote ndani ya ghala ikiwa ni pamoja na mizani na vitendea kazi vingine havina kasoro za kiufundi na pale zitakapobainika kuzirekebisha haraka iwezekanavyo.

(viii) Kuhakikisha ghala lina miundombinu yote muhimu inayofanyakazi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kila siku katika ghala kama maji, umeme na choo.

(ix) Kuhakikisha ghala lina watumishi wenye weledi wa kutosha kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za ghala.

### 4.8 WANUNUZI/WAFANYABIASHARA/MAWAKALA.

Wanunuzi watakaotambuliwa na mwongozo huu ni wafanyabiashara binafsi wenye leseni za biashara pamoja na makampuni au mashirika binafsi/umma ya ndani/nje ya nchi yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi zilizopo. Wanunuzi hawa watatakiwa:-

(i) Kujisajili rasmi kama mnunuzi wa ufuta/mbaazi kwa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa kabla ya kuruhusiwa kushiriki kwenye minada.

(ii) Kusaini mkataba wa makubaliano wa kununua ufuta/mbaazi kwenye Chama kikuu husika kwa mujibu wa mwongozo huu.

(iii) Kulipia kinga ya ghamana (bid security) kulingana na mahitaji yake ya kununua ufuta kama ilivyooneshwa kwenye **jedwali na.4: mchanganuo wa kinga za dhamana.**

(iv) Kulipia vibali mbalimbali kulingana na sheria ndogo za halmashauri ya Wilaya husika.

(v) Kuwasilisha zabuni za ununuzi ufuta/mbaazi eneo la mnada kuanzia saa 2.00 asabuhi hadi saa 06.00 mchana.

(vi) Kulipia ushuru wa Halmashauri ya wilaya **(3% ya bei ya Soko)** moja kwa moja katika akaunti ya Halmashauri.

(vii) Kuhakisha anatoa mzigo wake kwa wakati mara anapomaliza kulipa na kabla ya mnada mwingine kufanyika.

(viii) Kuhakikisha analipia mzigo alioshinda kwenye mnada ndani ya siku nne (4) za kazi.

**N.B. Mnunuzi hataruhusiwa kushiriki mnada mwingine kama hajamaliza kufanya malipo ya fedha za ufuta/mbaazi alizoshinda mnada uliyopita.**

(vi) Kuhakikisha ana vibali husika vya usafirishaji kutoka katika ngazi zote zinazohusika kabla ya kusafirisha ufuta/mbaazi kutoka ghala kuu.

(vii) Kuhakikisha analipa tozo zote kulingana na mwongozo kabla hajachukua mzigo kutoka kwenye ghala kuu.

(viii) Kuzingatia sheria, kanuni na miongozo yote ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, taasisi za fedha na mamlaka nyingine za serikali.

(ix) Kutoa ufuta walioshinda kwenye mnada katika ghala husika kwa mujibu wa mwongozo Namba 9 wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala sekta ndogo ya ufuta – TOLEO Na. 3.{Chini ya kifungu cha 6 (k,l,m na o) cha sheria Namba 10/2005 na kifungu cha 6 (n) cha sheria Namba 3/2015}

## 4.9 WAKALA WA VIPIMO.

(i) Kuhakikisha mizani zote zitakazotumika kupimia uzito wa ufuta/mbaazi ghafi kwa msimu 2021 zimekaguliwa.

(ii) Kutoa msaada wa kitaalamu juu ya mizani pale itakapohitajika.

(iii) Kufanya ukaguzi wa mizani mara kwa mara kipindi cha makusanyo.

(iv) Kuwawajibisha kwa mujibu wa sheria kwa wanaokiuka tarabu na sheria.

## 4.10 BENKI KUU YA TANZANIA (BOT)

(i) Kusimamia benki zote za biashara ili kuhakikisha malipo kutoka benki moja kwenda nyingine yafanafanyika kwa wakati.

(ii) Kuhakikisha taratibu zote za uhamishaji wa fedha zinafuatwa.

(iii) Kusimamia taratibu na kuhakikisha nchi inapata fedha za kigeni stahiki za mauzo ya ufuta haraka iwezekanavyo.

(i) Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu

(ii) Kutoa ushauri wa namna bora za kuboresha mifumo ya malipo ya kibenki na taratibu za kufuatwa na wadau mbali mbali endapo kutatokea changamoto.

## 4.11 TAASISI ZA FEDHA.

Majukumu ya taasisi mbalimbali za kifedha yatakuwa kama ifuatavyo;

(i) Kuhakiki taarifa za malipo kabla ya kuanza kuingiza kwenye akaunti husika.
(ii) Kufanya malipo ya wakulima kwa wakati mara tu baada ya kuwasilishwa na chama kikuu.
(iii) Kuhamasisha wakulima kufungua akaunti na kutoa taarifa kwa wakulima ili wahuishe akaunti mfu au zinazoelekea kusinzia kabla ya msimu kuanza.
(iv) Kuhakikisha miamala inayofanyika inaonesha majina ya walipwaji.
(v) Kutoa taarifa za malipo chama kikuu kwa ajili ya rejea ya baadae.
(vi) Kutoa taarifa za malipo yaliyokwama (Rejects) kwa chama kikuu kwa wakati.
(vii) Kupokea taarifa za malipo kutoka kwa timu ya uhakiki kabla taarifa hizo hazijawasilishwa chama kikuu kwa ajili ya malipo.
(viii) Kuhakikisha benki husika zina fedha za kutosha wakati wote wa kipindi cha ununuzi wa mazao ya ufuta na mbaazi.
(ix) Kuhakikisha fedha za wakulima/vyama vya ushirika zinazostahili kuhamishwa kutoka benki moja kwenda benki nyingine zinahamishwa kwa wakati.

## 4.11 WASAFIRISHAJI.

(i) Kuhakikisha wanakibali cha usafirishaji kutoka UNIONS na wawe wameweka kinga ya dhamana isiyopungua sh.10,000,000.00
(ii) Kuhakikisha wanakuwa na nyaraka zote za mzigo wanaosafirisha.
(iii) Kuhakikisha anasafirisha mzigo kwa muda uliopangwa.
(iv) Kuingia mikataba ya usafirshaji na vyama husika.
(v) Kuhakikisha taratibu za usafirishaji wa mazao zinafuatwa.

## 4.12 KAMATI ZA USALAMA MKOA/WILAYA

(iii) Kuhakikisha ulinzi unakuwepo popote pale ufuta/mbaazi unapokuwa au kusafirishwa ndani ya Mkoa

(iv) Kufanya doria usiku na mchana kwenye vizuizi vyote ndani ya Mkoa

(v) Kuhakikisha taratibu nyingine zote zilizoainishwa zinafuatwa kulingana na mwongozo huu.

(vi) Kuwachukulia hatua wote watakaokiuka utekelezaji wa mwongozo huu.

## 4.13 BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA

(i) Kutambua ghala kuu na kutoa mapendekezo ya kisheria.

(ii) Kutoa leseni kwa watunza ghala kuu kwa mujibu wa sheria ya stakabadhi za ghala.

(iii) Kufuatilia watunza ghala kuu wote kuhakikisha wanapokea ufuta/mbaazi na kuhifadhia kwa mujibu wa taratibu na sheria.

(iv) Kuhakikisha watunza ghala wanaingiza taarifa za mapokezi na utoaji wa ufuta/mbaazi ghalani kwenye mfumo kwa wakati.

(v) Kuhakiki taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo na watunza ghala ni sahihi.

(vi) Kutoa ushauri ili kuboresha mfumo huu.

(vii) Kutatua migogoro pale inapotokea kati ya waendesha ghala na wadau wengine kwa mujibu wa sheria kanuni na miongozo iliyopo.

(viii) Kutoa elimu ya kutosha kwa wadau kuhusu viwango vya ubora wa mazao pamoja na vifungashio.

(ix) Kuainisha viwango na vigezo vya aina ya vifungashio na ubora kwa zao la ufuta/mbaazi.

## 4.14 SOKO LA BIDHAA TANZANIA

Katika mwongozo huu soko la bidhaa Tanzania (TMX) litakuwa na majukumu yafuatayo kama wadau wa kikao wataridhia kuuza mazao yao kupitia minada ya mitandaoni.

i. Kuandaa utaratibu mzima wa shuguli za minada
ii. Kutoa elimu ya kutosha kwa makundi yote ya wadau kuhusu mfumo unavyofanya kazi kabla ya msimu wa ununuzi haujaanza.
iii. Kutoa elimu ya viwango vya ubora wa bidhaa inayotakiwa na wanunuzi.
iv. Kutafuta masoko bora kwa mazao ya ufuta na mbaazi.
v. Kutoa miongozo ya namna minada ya mitandaoni inavyoendeshwa.

### 4.15 WIZARA YA KILIMO

Wizara ya kilimo itakuwa na mjukumu yafuatayo katika huu mwongozo;

i. Kufuatilia mchakato mzima wa ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya ufuta na mbaazi.
ii. Kuhakikisha wakulima wa mazao ya mbaazi na ufuta wanafaidika kwa kulima kilimo biashara
iii. Kutatua migogoro kati ya wadau endapo kama ngazi ya mkoa itakuwa imeshindikana.
iv. Kushauri namna bora ya uzalisha na uuzaji wa mazao ya ufuta na mbaazi ili yawe na tija bora kwa mkulima na serikali kwa ujumla.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAANDALIZI NA MAHITAJI KATIKA MSIMU 2021

Katika msimu wa ufuta na mbaazi wa mwaka 2021 maandalizi ya msimu yanaendelea kulingana na mahitaji na mapendekezo ya wadau mbali mbali wa mkoa na nje ya mkoa.

### 5.1 UKUSANYAJI WA UFUTA NA MBAAZI GHAFI

Ukusanyaji wa ufuta na mbaazi utahusisha mambo yafuatayo; ufuta/mbaazi kutoka kwa mkulima na kupokelewa chama cha msingi, usafirishaji wa ufuta/mbaazi kutoka chama cha ushirika cha msingi kwenda ghala kuu, upokeaji na utunzaji wa ufuta/mbaazi katika ghala kuu.

i. Mkulima anawajibu wa kukusanya Ufuta/mbaazi shambani, kukausha vizuri na kuuchambua kabla ya kuupeleka kwenye Chama chake cha Msingi.
ii. Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kushirikiana na Maafisa ugani kitakagua Ufuta/mbaazi wa Mkulima kama vimekauka, na haujachanganywa na kitu chochote kisichokuwa Ufuta/mbaazi kabla ya kuupokea.
iii. Ufuta/mbaazi ghafi inatatakiwa kupimwa uzito kwa kutumia mzani uliohakikiwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo na Mizani (WMA) kwa mwaka 2021.
iv. Chama cha ushirika cha msingi kitatakiwa kumpatia mkulima stakabadhi yenye kuonesha kiasi cha uzito, jina la mkulima, akaunti namba, iliyosainiwa na karani pamoja na mjumbe.
v. Chama cha ushirika cha msingi kitatakiwa kufungasha Ufuta/mbaazi kwenye viroba vyenye ubora vilivyohidhinishwa. Aidha, uzito wa Ufuta/mbaazi ghafi katika kila gunia na unapaswa kuwa Kilo Hamsini (50).
vi. Mkulima/mtu yeyote haruhusiwi kununua Ufuta/mbaazi na kwenda kuuza kwenye chama cha msingi, endapo atathibitika kutenda kosa hilo atawajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi.
vii. Vyama vya msingi vitatakiwa kutunza takwimu sahihi za makusanyo na taarifa mbalimbali za msimu na kutoa taarifa hizo kwa wadau pale inapohitajika.

### 5.2 VIFUNGASHIO VYA UFUTA NA MBAAZI GHAFI

Vifungashio vya ufuta ghafi ni muhimu sana kwenye mauzo ya ufuta/mbaazi kwani ndio vinatambulisha ufuta wa nchi yetu sehemu mbalimbali duniani.

i. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala zitakuwa na jukumu la kuainisha aina ya vifungashishio vya mazao ya ufuta na mbaazi kwa mujibu wa viwango vya ubora vinavyotambuliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
ii. Vifungashio vipya na vilvyo hakikiwa tu ndivyo vitakavyotumika kufangashia mazao ya ufuta na mbaazi
iii. Chama cha Ushirika cha Msingi kitapaswa kuandika namba yake ya usajili kwenye viroba vyote vitavyotumika kwa kufuata utaratibu uliowekwa kabla ya kupelekwa ghala kuu.
iv. Chama cha Ushirika cha Msingi kitatumia viroba na kamba kwa ajili ya kufungasha ufuta uliochambuliwa kutoka kwa Mkulima aliyetoka katika chama hicho.
v. Chama kikuu kitahusika na kununua na kusambaza viroba na kamba kwenye vyama vya msingi.
vi. Chama kikuu kitahusika na usambazaji wa vitabu kwenye AMCOS.

## 5.3 UPOKEAJI NA UTUNZAJI WA UFUTA NA MBAAZI GHAFI GHALA LA AMCOS/KUU

i. Ghala la AMCOS litatakiwa kupokea ufuta na mbaazi ghafi katika ubora unaokubalika kwa kiwango cha **Bila Daraja 'BD'**
ii. Ghala la AMCOS wanapaswa kupokea viroba vya kuhifadhia ufuta/mbaazi vyenye jina la chama kikuu na namba ya usajili wa chama cha ushirika cha msingi husika.
iii. Mtunza ghala (ghala kuu) anatakiwa kuhifadhi na kutoa ufuta/mbaazi kwa mnunuzi husika ukiwa katika ubora na kiasi kama alivyozipokea kutoka kwa chama cha msingi.
iv. Mtunza ghala (ghala kuu) anatakiwa kuingiza taarifa za ufuta/mbaazi ghafi ulioingia ghalani kila siku kwenye mfumo wa kieletroniki wa Bodi ya Stakabadhi za Ghala zinazohusiana na kiasi cha uzito, idadi ya gunia, na mmiliki kwa wakati.
v. Mtunza ghala na chama kikuu cha ushirika wataandaa ***"sales catalogue"*** ambayo itatumika kwenye minada.

### 5.4. USAFIRISHAJI WA UFUTA NA MBAAZI KWENDA GHALA KUU

(i) Kulingana na mfumo wa stakabadhi ghalani/mnada baada ya ufuta/mbaazi kuwa vimekusanywa katika vyama vya msingi AMCOS vitatakiwa kusafirishwa hadi ghala kuu kwa ajili ya hatua ya mnada.

(ii) Chama cha msingi kitasafirisha ufuta/mbaazi kwenda ghala kuu kwa kutumia wasafirisha waliohidhinishwa na chama kikuu.

(iii) Mnunuzi atawajibika kulipa gharama za usafirishaji baada ya kushinda mnada.

(iv) Chama cha msingi kwa kushirikiana na Afisa Ushirika wa Halmshauri husika watashirikiana katika kukokotoa gharama za usafirishaji.

(v) Viwango vya usafirishaji vitakavyotumika itakuwa ni vile tu vilivyopitishwa kwenye vikao vya wadau.

(vi) Kwa sehemu korofi vyama vya msingi kupitia kwa Afisa ushirika wa halmashauri husika wawasiliane na ofisi ya mkuu wa mkoa kwa maelekezo zaidi.

**NB: Gharama za usafiri zitategemea hali halisi ya umbali na miundombinu ya barabara.**

### 5.5. UPATIKANAJI WA VIBALI VYA KUNUNUA UFUTA GHAFI

i. Mnunuzi atakayenunua ufuta/mbaazi ghafi katika msimu wa mauzo wa 2021 atatakiwa awe amesajiliwa na kupata kibali cha ununuzi inayotolewa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa.

ii. Mnunuzi mwenye Leseni/kibali cha kununua Ufuta/mbaazi ghafi kilichotolewa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa katika msimu wa 2021 anatakiwa kununua ufuta/mbaazi ghafi ndani ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

iii. Mnunuzi atatakiwa kuzingatia masharti na vigezo vya mnada wa mauzo ya Ufuta/mbaazi ghafi kama yalivyotolewa na kupitia vyama vikuu.

iv. Mnunuzi atatakiwa kuzingatia masharti ya leseni yake na Tozo zilizokubalika kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na taratibu zilizowekwa kupitia vikao vya wadau wa zao la ufuta Mkoa.

### 5.6. UENDASHAJI WA MINADA YA UFUTA NA MBAAZI GHAFI MWAKA 2021

i. Vyama Vikuu vya Ushirika vitaandaa ratiba itakayoonesha tarehe, muda na mahali pa kufanyia Minada na kuwatangazia wadau wote wanahusika.

ii. Mnunuzi atatakiwa kufika na kuwasilisha zabuni yake iliyofungwa kwa lakiri (**Seal**) kwenye sanduku la zabuni siku ya mnada kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 06.00 mchana.

iii. Kwa watumishi kutoka mashirika au makampuni ya ununuzi watakaokuja kuwasilisha barua za zabuni za ununuzi wa ufuta/mbaazi kwenye minada watapaswa kuonesha kitambulisho halali cha kampuni/shirika kinachotambuliwa na mnunuzi husikakabla ya kutumbukiza barua.

iv. Mnunuzi, kampuni au mashirika yatakayohitaji kununua ufuta/mbaazi kwa kuwatumia mawakala wakati wa uendeshaji wa minada, watapaswa kufanya yafuatayo.

    a. Kutoa taarifa kwa uongozi kwa chama kikuu husika. Mawakala ambao hawajatambulishwa barua zao za zabuni hazitapokelewa.
    b. Aidha, mawakala watapaswa kuwasilisha barua rasmi za utambulisho zilizosainiwa kutoka kwa mnunuzi binafsi, kampuni au shirika ambazo zitahakikiwa na chama kikuu husika.

i. Funguo ya sanduku zitakuwa mbili ambapo ufunguo mmoja utakuwa ofisi ya mkuu wa Mkoa na ufunguo wa pili ofisi ya chama kikuu cha ushirika.

ii. Mnada utafanyikia sehemu ya wazi ambapo wakulima waliopo katika eneo husika pamoja na wadau wengine watashiriki.

iii. Sanduku la zabuni litafunguliwa mbele ya wakulima baada ya muda kuisha wa kupokea barua za maombi chama kikuu cha ushirika kitatakiwa kutoa taarifa ya malipo ya ufuta ulionunuliwa katika mnada uliotangulia.

iv. Ufunguzi wa zabuni utakuwa wa wazi ambapo pamoja na taarifa nyingine itasomwa bei ya zabuni uwazi, na mwenyekiti au makamu mwenyekiti wa chama kikuu ndio atakuwa mwenyekiti wa mnada huo.

v. Washiriki wa mnada watakuwa ni wakulima na wanachama wa vyama vya ushirika, Wanunuzi, wawakilishi kutoka sekretariet ya Mkoa, Mamlaka za serikali za mitaa, Vyama vya Ushirika na viongozi wengine toka taasisi mbali mbaili pamoja viongozi waalikwa.

## 5.7 TARATIBU ZA MINADA

(i) Mwendesha ghala atahakikisha anatoa taarifa za mapokezi ya ufuta/mbaazi kutoka AMCOS na kuziwasilisha chama kikuu kwa ajili ya kuandaa sale catalogue

(ii) Chama kikuu kitapokea stakabadhi (ware house receipt) kutoka kwa AMCOS pamoja na taarifa ya mapokezi ya mwendesha ghala kila baada ya siku 6

(iii) Minada itafanyika kila jumamosi na jumapili ili kuhakikisha malipo yanafanyika yanafanyika siku za kazi.

(iv) Malipo kwa wanunuzi walioshinda yatafanyika ndani ya siku mbili za kazi.

(v) Baada ya kukamilisha malipo mnunuzi/mfanyabiashara atapaswa kutoa mzigo ndani ya siku saba (7) kutoka tarehe ya **hati ya kutolea mzigo (release order).**

(vi) Wafanya biashara ambao hawajakamilisha malipo hawataruhusiwa kuchukua mzigo wala kushiriki katika mnada unaofuata, hali kadhalika kwa wale ambao hawajatoa mzigo wao baada ya kuulipia watashughulikiwa kwa sheria inayosimamia maghala.

(vii) Mnunuzi atanunua ufuta/mbaazi ghafi kulingana na takwimu ya mzigo uliokusanywa na kutangazwa na Vyama Vikuu kupitia **sales catalogue**.

(viii) Maombi yote ya ununuzi wa ufuta/mbaaazi ghafi yatatumwa kwa chama kikuu.

(ix) Taarifa za mauzo (**Sales catalogue**) zitaandaliwa na Vyama vikuu na zitaonesha kiasi cha mzigo uliopo na ubora wake, jina la ghala, wilaya, pamoja na AMCOS

(x) Taarifa za minada zitatolewa kwa wanunuzi/wafanyabiashara siku mbili kabla ya mnada.

(xi) Barua za maombi kutoka kwa wanunuzi zitahifadhiwa kwenye sanduku maalumu la tenda mpaka muda wa ufunguzi.

(xii) Maombi yafungwe kwenye bahasha yenye LAKIRI (sealed).

(xiii) Muda wa kuwasilisha maombi ni kuanzia saa mbili asubuhi **(2:00 asbh)** hadi saa sita **(06:00 mchana).**

(xiv) Mnunuzi atapewa hati ya kutoa mzigo (**release warranty**) mara tu baada ya kukamilisha malipo.

(xv) Mwenyekiti wa mnada atatakiwa kuwahoji wakulima endapo wanakubaliana na bei zilizopo mnadani, iwapo bei hizo hazikubaliki basi mzigo utauzwa kwa mara nyingine tena mnada unaofuata.

(xvi) Mwombaji mwenye bei kubwa ndiye atakayetangazwa mshindi kwenye mnada.

(xvii) Endapo bei za wanunuzi zitalingana, aliye wasilisha maombi mapema ndie atakayetangazwa mshindi na kununua mzigo.

(xviii) Ufuta/mbaazi vitarudi mnadani endapo:

- Utakosa mnunuzi.
- Mnunuzi atashindwa kulipa kwa wakati.

**NB: Utaratibu wa minada ya mtandaoni unaosimamiwa na soko la bidhaa Tanzania utatumika endapo wadau wataridhia kutumika kwa mfumo huo.**

## 5.8 TARATIBU ZA MALIPO

(i) Malipo yote yatafanyika kupitia taasisi za fedha kwa ngazi zote (Wanunuzi, Vyama Vikuu, AMCOS na wakulima)

(ii) Wanunuzi watalipa fedha za AMCOS moja kwa moja kwenye akaunti za vyama vikuu.

(iii) Maandalizi ya malipo yatafanyika kwenye vituo vya malipo (payment centres). Vilivyopo kwenye kila halmashauri.

(iv) Vyama vikuu vitawajibika kuandaa miamala ya malipo ikiwa ni pamoja na tozo zote na kuziingiza kwa kila mdau. **NB:** Aidha UNIONS zitaingiza fedha za wakulima moja kwa moja kwenye akaunti zao na AMCOS zitaingiziwa fedha za ushuru wao tu.

(v) AMCOS, Maafisa Ushirika pamoja na Vyama vikuu vitahakiki malipo yote kabla ya kupelekwa benki.

(vi) Taasisi za fedha zihakiki miamala ya malipo kabla ya kuingiza kwenye akaunti za wakulima pamoja na wadau wengine.

## 5.9 TARATIBU ZA UTOAJI WA UFUTA NA MBAAZI GHALANI

(i) Mnunuzi anatakiwa kuwasilisha hati ya kutolea mzigo (release order) kutoka chama kikuu cha Ushirika.

(ii) Ufuta/mbaazi inatakiwa kuwa vimedaradishwa (standardized) kwenye viroba ukiwa na kilo 50.

(iii) Kiwango cha upungufu katika vifungashio hautakiwi kupungua zaidi ya 1.3% kwa ufuta/mbaazi uliyohifadhiwa siku zisizozidi 90 kwa mujibu wa mwongozo na.10 wa mfumo wa stakabadhi za ghala.

(iv) Mnunuzi aliyeshida tenda ya kununua ufuta/mbaazi anatakiwa kutoa ufuta/mbaazi ghalani ndani ya siku 7 tangu tarehe ya mnada.

(v) Baada ya siku 7 kupita tangu ufuta ununuliwe mnadani, mnunuzi anachajiwa **sh.1/=** kwa kilo kwa kila siku itakayokuwa inaongezeka. Hivyo mnunuzi anatakiwa baada tu ya kununua ufuta/mbaazi anatakiwa kufuatilia taratibu zote zilizoainishwa katika mwongozo huu ili kuepukana na usumbufu huo.

(vi) Gharama ya kuhifadhia ufuta/mbaazi italipwa na mnunuzi kabla ya kutoa mzigo wake.

(vii) Mtunza ghala atawajibika na upotevu/upungufu wa ufuta/mbaazi ghalani kwake.

## 5.10 KUANZA KWA MSIMU WA UNUNUZI WA UFUTA NA MABAAZI

### 5.10.1 UNUNUZI WA ZAO LA UFUTA

Kikao cha wadau kilichofanyika tarehe 4 Mei 2021 ukumbi wa mikutano ofisi ya Mkuu wa Mkoa wadau walikubaliana mnada wa kwanza ufanyike tarehe 29 Mei 2021.

### 5.10.2 UNUNUZI WA ZAO LA MBAAZI

Kabla ya kuanza kwa ununuzi wa zao la mbaazi mkoa utatoa maelekezo ya tarehe ya kuanza kwa ununuzi sambamba na maelekezo mengine kuhusu maandalizi.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 UDHIBITI NA USULUISHI WA MIGOGORO

### 6.1 UDHIBITI WA UTOROSHAJI/UDANGANYIFU NA UNUNUZI HOLELA WA UFUTA/MBAAZI

Kamati za Usalama **(KU)** kwa ngazi zote (Mkoa, Wilaya) pamoja na Kikosi kazi (task force) zitahusika na udhibiti wa utoroshaji na uuzaji holela wa ufuta/mbaazi. Aidha, sheria zilizopo zitatumika kwa wale wote watakaouza au kununua ufuta/mbaazi kiholela sambamba na wale watakaotorosha.

### 6.2 ADHABU KWA MFANYABISHARA ATAKAYEKWEPA KULIPA TOZO

Halmashauri zitatumia sheria zao ndogo za ushuru wa mazao ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, (sura namba 290 ya Sheria za Tanzania) ambayo kwa marekebisho yake ya Mwaka 2017 yaliyofanywa na Sheria ya Fedha, adhabu kwa kukiuka taratatibu na matakwa ya Sheria hiyo ni faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili.

> **Angalizo:** Hii si mbadala wa kulipa tozo husika hivyo, mbali na faini hizo anatakiwa alipe tozo halisi alizotakiwa kuzilipa.

### 6.3 MNUNUZI KUCHELEWA KULIPA AU KUTOLIPA.

Kwa wanunuzi ambao watashindwa kulipia fedha za mauzo ya ufuta/mbaazi kwa wakati kulingana na taratibu za mwongozo huu, watajibika na yafuatayo:-

(i) Kinga ya dhamana aliyoweka itatumika kufidia hasara itakayojitokeza baada ya mnunuzi kuchelewa au kutolipa kwa wakati.

(ii) Uwepo mkataba utakao kuwa na maelekezo na masharti ikiwa ni pamoja na mnunuzi kutakiwa kulipa hasara itakayojitokeza baada ya ufuta/mbaazi huo kuuzwa kwa mara ya pili.

(iii) Mhe. Mkuu wa Mkoa na waheshimiwa Wakuu Wilaya wanaweza kutumia kifungu cha 7 na 15 vya Sheria ya Tawala za Mikoa inayowapa mamlaka ya kuchukua hatua kwa wale wanaosababisha uvunjifu wa amani.

## 6.4 UDANGANYIFU UNAOFANYWA NA MAKARANI AU WATENDAJI WA AMCOS.

(i) Sheria ya Vyama vya Ushirika namba 6 ya mwaka 2013 kifungu cha 129(1) na (2) vitatumika kwa kiongozi/mwajiriwa wa chama cha Ushirika atakae eneda kinyume na matakwa au makubaliano na chama husika.

## SEHEMU YA SABA

### 7.1 MAPENDEKEZO YA TOZO

Kamati inapendekeza tozo zifuatazo katika ununuzi wa zao la ufuta msimu huu:-

***Jedwali Na.3: Aina za tozo katika ununuzi wa ufuta msimu 2021***

| NA. | AINA YA TOZO | TOZO KWA MKULIMA (Tshs) | TOZO ZINAZOLIPWA NA WANUNUZI (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | UNIONS | 15.00 | |
| 2 | AMCOS | 60.00 | |
| 3 | Maendeleo ya elimu Halmashauri | 25.00 | |
| 4 | Utafiti – TARI Naliendele | 1.00 | |
| 5 | Mfuko wa elimu mkoa | 2.00 | |
| 6 | Vituo vya malipo (Payment centers) | 2.00 | |
| 6 | Ushuru wa Halmashauri | | 3% ya bei ya mnada |
| 7 | Vifungashio | | 19.00 |
| 8 | Usafirishaji | | 55.00 |
| 8 | Mtunza ghala | | 38.00 |
| | **JUMLA** | **105.00** | |

***Jedwali Na.4: Aina za tozo katika ununuzi wa mbaazi msimu 2021***

| NA. | AINA YA TOZO | TOZO KWA MKULIMA (Tshs) | TOZO ZINAZOLIPWA NA WANUNUZI (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | UNIONS | 12.00 | |
| 2 | AMCOS | 33.00 | |
| 3 | Maendeleo ya elimu Halmashauri | 13.00 | |
| 5 | Mfuko wa elimu mkoa | 2.00 | |
| 6 | Ushuru wa Halmashauri | | 3% ya bei ya mnada |
| 7 | Vifungashio | | 19.00 |
| 8 | Usafirishaji | | 55.00 |
| 8 | Mtunza ghala | | 38.00 |
| | **JUMLA** | **60.00** | |

## 7.2 KINGA YA DHAMANA

Kila mnunuzi anatakiwa kuweka kinga ya dhamana ya zabuni kwa fedha taslim (Bid security) kabla ya kupata kibali cha kununua ufuta/mbaazi katika akaunti maalum kwenye chama kikuu cha Ushirika na kinga hiyo itarejeshwa baada ya msimu kumalizika kwa viwango vifuatavyo:-

**Jedwali Na.4. Mchanganuo wa kinga za dhamana**

| Na. | Kiasi cha ufuta/mbaazi kwa mnada (Kgs) | Kiasi cha fedha (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | 50,000 – 100,000 | 10,000,000/= |
| 2 | 101,000 – 500,000 | 30,000,000/= |
| 3 | 501,000 – 1,000,000 | 50,000,000/= |
| 4 | 1,001,000 – nakuendelea | 75,000,000/= |

**NB:**

1. Mnunuzi haruhusiwi kununua zaidi ya kiasi kile alichowekea kinga ya dhamana kwa ujumla katika mnada.
2. Fedha za kinga ya dhamana zitaingizwa kwenye mojawapo ya akaunti za pamoja (Collections accounts) zilizopo chama kikuu cha Lindi mambao Ltd na Runali ltd.

===============**MWISHO**==============